# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Septemba,2025 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022**

# SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI



***Bw.Jimson Mhagama-Mkurugenzi Mtendaji-Same***

# *Tushiriki Uchaguzi Mkuu kwa Amani na Utulivu*

***Oktoba 29, 2025 Watanzania tunatarajia kushiriki Uchaguzi Mkuu ambao hufanyika hapa nchini kila baada ya miaka mitano ukijumuisha vyama vingi vya siasa.***

***Kila Mtanzania ana wajibu wa kujitokeza kwenye kushiriki zoezi la uchaguzi iwapo tu alitumia vema nafasi yake ya kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga kura .***

***Sifa ya kwanza ya kushiriki uchaguzi Mkuu ni lazima mwananchi awe amejiandikisha kwenye Daftari la kudumu la wapiga kura na awe na kadi ha mpiga kura.***

***Iwapo unazo sifa za kupiga kura basi hakikisha unajitokeza kuchagua kiongozi atakayekuvusha kwa miaka mitano ijayo, kiongozi ambaye atakutumikia vema.***

***Ili kumtambua kiongozi bora atakayekuvusha kwa miaka mitano ijayo hakikisha unahudhuria mikutano ya kampeni na kusikiliza vema sera za wagombea na kupitia sera hizo utakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuchagua kiongozi bora.***

***Ili kufanikisha zoezi la uchaguzi tayari Serikali imeshatangaza kuwa Oktoba 29,2025 ni siku maalum ya kushiriki uchaguzi hivyo ni siku ya mapumziko, na mapumziko haya ni ya kumwezesha kila mtanzania kuweza kushiriki uchaguzi Mkuu.***

***Hakikisha inapofika siku ya uchaguzi unaelekea kwenye kituo ulichojiandikisha ukiwa na kitambulisho chako cha mpiga kura na kwenda kumchagua Rais,Mbunge na Diwani unayemtaka.***

***Fuata utaratibu wote utakaokuta kituoni na unapomaliza kupiga kura hakikisha unaondoka eneo la kupigia kura kwa amani na utulivu na hairuhusiwi kufanya mkusanyiko wowote kwa lengo la kusubiri matokeo ama vinginevyo.***

***Wilaya yetu ya Same ina jumla ya Vituo 495 vya kupigia kura ambapo vituo 213 vinavyotarajiwa kutumiwa na***

*wapiga kura 74110 vipo Jimbo la Jimbo la Same Mashariki na vituo 282 vinavyotarajiwa kutumiwa na wapiga kura 100316 vipo Jimbo la Same Magharibi.*

*Unapokwenda kupiga kura hakikisha unaepuka mambo yafuatayo kwani hayaruhusiwi siku ya uchaguzi:-*

- *Kufanya Kampeni*
- *Kuvaa sare au alama ya chama chochote cha siasa.*
- *Kuendelea kuwepo eneo la kituo cha kupigia kura hata baada ya kumaliza kupiga kura*
- *Kutumia simu ya kiganjani uwapo kwenye kituo cha kupiga kura*
- *au kuhesabia kura.*
- *Kutoa lugha ya matusi*

*Nawatakia kila la kheri katika kushiriki Uchaguzi Mkuu 2025*



# RAS KILIMANJARO APONGEZA UTEKELEZAJI MIRADI SAME



***Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Kiseo Nzowa (katikati)alipotembelea Shule ya Sekondari Misufini Goma,kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni,wengine kushoto ni Afisa Elimu Sekondari Bi.Neema Lemunge na Mhandisi wa Nzaro Jonathan.***

Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Kilimanjaro Bw. Kiseo Nzowa amepongeza utekelezaji wa Miradi Wilayani Same wakati alipofanya ziara ya siku moja ya kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa Wilayani Same.

Katika ziara hiyo RAS Nzowa alitembelea Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Amali ya Kihurio ambayo Ujenzi wake unagharimu Mil. 584.28 fedha kutoka Mradi wa SEQUIP na ujenzi wake umefikia asilimia 95.

Miradi mingine iliyotembelewa ni Mradi wa Bwalo la Chakula kwenye Shule ya Sekondari Ndungu ambao unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi mil. 195 ambapo kati ya fedha hizo Mil. 170 zimetoka Serikali Kuu na Mil 25 zimetokana na mapato ya ndani ya Halmashauri.

Katibu Tawala Nzowa alihitimisha ziara yake kwa kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Kidato cha tano na sita kwenye Shule ya Sekondari Misufini Goma ambao umegharimu Shilingi Milioni 389.4 kutoka SEQUIP.

Miradi yote iliyotembelewa ujenzi wake umekamilika kwa zaidi ya asilimia 95 ambapo Katibu Tawala aliipongeza Halmashauri kwa usimamizi mzuri wa Miradi na kuelekeza hatua ya umaliziaji kuhakikisha kuwa majengo yote yanawekwa sakafu ya marumaru(tiles).

"Naona Miradi hii ipo kwenye hatua za umaliziaji, hivyo hakikisheni inakamilika kwa wakati ili iweze kupokea wanafunzi mwakani" alisema Nzowa.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni aliishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya ya Same Miradi itakayowezesha wanafunzi wengi zaidi kujiunga na Elimu ya Sekondari pamoja na kunufaika na Elimu ya Amali (Ufundi).

## BODI YA PAMBA YAZAWADIA WAKULIMA NA MAAFISA KILIMO SAME



***Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Wambura Yamo (kushoto) akimkabidhi zawadi kwa Afisa Mifugo na Kilimo wa Kata ya Kisiwani Bi. Fatuma Sadalla (kulia ) ambaye amefanya vizuri katika uzalishaji wa zao la Pamba, nayetazama katikati ni Afisa Mifugo na Kilimo Wilaya Bw.Ninzari Idd, Zawadi hiyo***

***ilitolewa na Bodi ya Pamba  Tanzania baada ya Kata ya Kisiwani kutoa wakulima Bora wa Pamba.***

Bodi ya Pamba nchini (TCB)) imetoa zawadi ya majiko ya gesi kwa wakulima hodari wa Pamba Wilayani Same ambao wameweza kuzingatia kanuni za kilimo bora cha Pamba kilichowezesha uzalishaji wa zaidi ya kilo 1,500 kwenye ekari moja.

Bodi hiyo pia imetoa zawadi ya vitenge na kanga kwa maafisa Ugani Wilayani Same kama sehemu ya kutambua mchango wao katika kuongeza uzalishaji wa zao la Pamba.

Wakulima walionufaika na zawadi hizo ni Gabriel Mbwambo na Praise Mbwambo ambao wote wanatoka Kata ya Kisiwani na maafisa ugani waliopatiea zawadi ni Debora Mtati na Fatuma Sadala.

Akikabidhi zawadi hizo Afisa Kilimo kutoka Bodi ya Pamba Bw. Alphonce Ngawagala alisema utoaji wa zawadi ni motisha kwa Wakulima na maafisa ugani ili kuchochea ongezeko la uzalishaji wa Pamba hapa nchini.

"Bodi ya Pamba itaendelea kutoa zawadi kama motisha kwa wakulima wa pamba ili zao hili liweze kuzalishwa kwa wingi katika maeneo mengi wilayani Same na nchini kwa jumla"alisema Bw.Ngawagala na kuongeza kuwa mwaka jana Bodi hiyo ilikabidhi zawadi ya Trekta yenye thamani ya mil 55 kwa mkulima Gabriel Mbwambo baada ya kuibuka mkulima bora wa Pamba kwenye Kanda hii.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Wambura Yamo aliwapongeza Wakulima waliofanya vizuri msimu huu na kuwataka kuongeza jitihada ili zao la Pamba lienee maeneo mengi Wilayani Same."Uzalishaji wa Pamba unapoongezeka hata mapato ya serikali yanaongezeka kupitia ushuru wa mazao na Serikali inapoongeza mapato inaboresha utoaji wa huduma za kijamii.

## DC SAME AWATAKA WAFANYABIASHARA KUTOA RISITI ZA EFD.




*Mashine ya kutolea risiti za kielektronik za EFD*

Mkuu wa Wilaya ya Same, Mheshimiwa Kasilda Mgeni, amewataka wafanyabiashara kuendelea kutumia mashine za kielektroniki za kodi (EFD) ili kuhakikisha kila mteja anapata risiti ili kulinda mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Kasilda alitoa wito huo katika kikao cha Kamati ya Ushauri wa Kodi cha Wilaya, ambapo alisisitiza kuwa ni jukumu la kila mfanyabiashara kutoa risiti kwa kila mauzo anayofanya, huku akiwaasa wateja kudai risiti wanaponunua bidhaa.

"Tunatakiwa kuendelea kuwaelimisha wafanyabiashara kutumia mashine za EFD, kutoa risiti kwa wateja huku wateja wakisisitizwa kudai risiti wanaponunua bidhaa, ili kulinda mapato ya serikali yasipotee," alisema Mhe. Kasilda.

Akizungumza kwenye kikao hicho Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Wilaya ya Same, Eliapenda Mwanri, alieleza kuwa Taasisi hiyo

imefanikiwa kuvuka lengo la makusanyo la Shilingi bilioni 8.04 kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Mei 2025, ambapo walifanikiwa kukusanya bilioni 8.1.

Bw. Mwanri aliongeza kuwa mafanikio hayo yametokana na utoaji wa elimu kwa walipakodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na msisitizo wa matumizi ya mashine za EFD.

Kikao cha kisheria hufanyika mara mbili kwa mwaka ikiwa na lengo la kuangalia mwenendo wa makusanyo ya mapato katika Wiilaya na kuweka mikakati ya kuongeza ukusanyaji wa mapato.

## DED MHAGAMA AISHUKURU JAPAN KWA KUJENGA ZAHANATI



***Mwakilishi wa Balozi wa Japan nchini Bi.Chika Umetsu akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi na wananchi wa Suji wakati alipotembelea kukagua Mradi wa Zahanati ya Suji Malindi ambayo ujenzi wake umefadhiliwa na ubalozi wa Japan.***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Same Bw.Jimson Mhagama ameushukuru Ubalozi wa Japan hapa nchini kwa kutoa Milioni 281.3 kufadhili Ujenzi wa Zahanati ya Malindi iliyopo Kata ya Siku Wilayani hapa.

Mkurugenzi Mhagama ametoa shukrani hizo wakati mwakilishi wa Balozi wa Japan ambaye pia ni Mshauri wa Masuala ya Miradi kwenye Ubalozi wa Japan hapa nchini Bi.Chika Umetsu alipofika kutembelea Zahanati ya Malindi.

Ujenzi wa Zahanati ya Malindi umegharimu Jumla ya Shilingi Milioni 470.26 ambapo imejumuisha Ufadhili huo wa Japan kupitia Miradi wa Msaada wa kuwezesha Usalama wa wananchi wa Vijijini (Grant Assistance for Grassroots Human Security Project).

Ufadhili mwingine wa Shilingi Milioni 38.6 umetolewa wa Serikali Kuu kupitia Miradi wa maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (SRWSSP)

Halmashauri ya Wilaya ya Same kupitia fedha za mapato ya ndani ilichangia Shilingi Milioni 37.3 ambapo nguvu za wananchi ni Milioni 113.

Katika awamu ya kwanza ya ujenzi ufadhili huu umefanikisha Ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa Nje ambalo linajumuisha wadi ya mama,Baba na mtoto,huduma za uzazi,Ujenzi wa Choo cha matundu manne pamoja na ununuzi wa samani pamoja na Ujenzi wa Nyumba moja ya Mtumishi.

Awamu ya pili ambayo itakamilika Agosti mwaka imejumuisha Ujenzi wa kichomea taka,shimo la kutupa kondo la nyuma,shimo la majibu na sehemu ya kunawa mikono.
Zahanati ya Malindi imesajiliwa na imeshaanza kutoa huduma na tayari imeshahudumia wananchi zaidi ya 650O.



**WAFUGAJI WATAKIWA KUSHIRIKI ZOEZI LA UTOAJI WA CHANJO ZA MIFUGO**



***Afisa Mifugo Wilayani Same Herman Shayo akiwashiriki zoezi la uwekaji hereni za kielektronic kwa mifugo.***

Wafugaji Wilayani Same wametakiwa kutoa ushirikiano kwa maafisa mifugo wakati huu ambao kunafanyika zoezi la utoaji wa chanjo za mifugo zenye ruzuku ya Serikali ili kukinga mifugo na kuku dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Afisa Mifugo na kilimo Wilayani Same Bw.Ninzari Idd amesema zoezi hilo la chanjo ya Ruzuku linakwenda sambamba na zoezi la utambuzi wa mifugo kwa kuvishwa hereni maalumu za kielektroniki ili iweze kutambuliwa popote itakapokuwepo.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** katika juhudi za kuboresha uzalishaji wa mifugo hapa nchini alizindua kampeni ya Kkitaifa ya utoaji chanjo za mifugo zenye ruzuku ya Serikali tarehe 16 Juni 2025 Wilayani Bariadi (Simiyu).

Chanjo hizi ni dhidi ya **Homa ya Mapafu ya Ng'ombe** (CBPP) ambayo inatolewa kwa Tsh 500 kwa ng'ombe mmoja badala ya Tsh 1000 na kwa upande wa mbuzi, chanjo ya **Sotoka ya mbuzi** itatolewa kwa Tsh 300 kwa mbuzi mmoja badala ya Tsh 500 ya bei ya soko. Aidha chanjo ya kuku aina ya **Tatu moja** ambayo ni dhidi ya magojwa ya Ndui, Mafua na kideri yanayoathiri kuku inatolewa bure (bila malipo).

Bw.Ninzari amesema faida za kampeni hii ya kitaifa ya utoaji chanjo na utambuzi wa mifugo ni pamoja na kuboresha afya za mifugo na uzalishaji, kuwa na uhakika wa masoko ya mifugo ndani nan je ya nchi  na kuzuia wizi wa mifugo.

Zoezi la utoaji wa chanjo za mifugo Wilayani Same lilianza Julai 4, 2025 kwa utoaji wa chanjo aina ya **Tatu moja** kwa kuku dhidi ya magonjwa ya Ndui, Mafua makali na kideri/mdondo ambapo hadi mwanzoni mwa mwezi Oktoba 2025, jumla ya kuku **202,401** wamechanjwa na lengo ni kufikia kuku **220,000.**

Ambapo kwa upande wa Ng,ombe jumla ya Ng'ombe **24,364** wameshachanjwa na kuwekwa hereni za kielekroniki kati ya ng'ombe **130,000** wanaotarajiwa kuchanjwa katika Wilaya ya Same.

Mfugaji John Samweli Mamasita wa Kata ya Ruvu amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwaletea chanjo wa mifugo yenye ruzuku kwani imewapunguzia gharama hivyo itawezesha mifugo yote kuchanjwa.

Naye Mfugaji Yohana Kiroya ambaye anasema tayari mifugo yake imeshapatiwa chanjo na anaendelea na zoezi la uwekaji hereni za kielektronik ameishukuru Serikali kwa kuwapatia ruzuku ya Chanjo.

## WATAKIWA KUSAFISHA MAZINGIRA YANAYOWAZUNGUKA



***Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same Dk. Alex Alexander (kulia) akishiriki na wananchi kufanya usafi kwenye maadhimisho ya siku ya usafi Duniani  ambayo huadhimishwa Septemba 20 ya kila mwaka.***

Afisa Afya wa Wilaya ya Same Bi. Yuster Malisa amewataka wananchi Wilayani Same kuwa na tabia ya kusafisha mazingira kwenye maeneo wanayoishi ili kuhakikisha yanakuwa safi muda wote.

Ametoa wito huo wakati akizungumza na wananchi walioshiriki kufanya usafi siku ya Usafishaji Duniani ambayo huadhimishwa Septemba 20 ya kila mwaka ambapo alisema wananchi hawana tabia ya kusafisha mazingira yanayozunguka makazi na biashara zao.

"Kila mwananchi anapaswa kuhakikisha kuwa mazingira yanayomzunguka yaani mita tano kila upande unaozunguka nyumba au biashara yake unakuwa safi" alisisitiza Afisa Afya.

Aidha Bi, Yuster ameonya tabia ya baadhi ya wananchi na wafanyabiashara ambao wana tabia ya kutupa taka kwenye mitaro ya maji ya mvua ambapo alisema atakayebainika kufanya hivyo atatozwa faini.

"Kila mmoja asimame imara kuhakikisha kwamba eneo analoishi ama kufanyia biashara linakuwa safi ili tuweze kuepuka magonjwa ya mlipuko"alisema Afisa afya

## WANANCHI TOENI USHIRIKIANO KWENYE USAJILI WA NYUMBA



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama Bw. amewataka wananchi kutoa ushirikiano kwa watumishi wanaopita kwenye maeneo yao kwaajili ya kufanya usajili wa majengo/nyumba zilizopo kwenye Wilaya ya Same.

Bw.Mhagama ametoa wito huo wakati akizungumzia umuhimu wa zoezi hilo ambapo alisema litawezesha ongezeko la mapato ya Halmashauri na hivyo kuiwezesha Halmashauri kuweza kutoa vema huduma za kijamii kwenye maeneo mbalimbali.

"Tunaendelea na zoezi la usajili wa makazi kwenye vijiji vyote 100 vya Wilaya ya Same hivyo tunahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi ili kuweza kukamilisha zoezi hili kwa ufanisi" alisema Mhagama.

Mratibu wa Kodi ya Majengo na Mabango willayani Same Bw.Jackson Komentian amesema zoezi hilo linafanyika kuwa kuingiza nyumba hizo kwenye mfumo maalum wa ODK na lengo ni kurahisisha ukusanyaji wa kodi ya jengo katika nyumba ambazo hazina umeme.

Itakumbukwa kuwa Serikali ilihamishia ukusanyaji wa Kodi ya Jengo kwenye huduma ya ambapo nyumba zote zenye umeme kodi hiyo hulipwa kupitia malipo ya luku huku nyumba zisizo na umeme zikibaki bila kulipa kodi hiyo.


Amesema lengo ni kuhakikisha kuwa nyumba zote zinasajiliwa ili zile ambazo hazina umeme Halmashauri iweze kukusanya kodi hiyo.

"Usajili wa Nyumba unafanyika kwenye mfumo na tayari tayari watendaji wa Kata na Vijiji zaidi ya 120 tumeshawapatia Mafunzo ya usaji na zoezi la usaji limeshaanza" alisema

Amesema lengo ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ili wananchi waweze kupatiwa huduma bora za kijamii ambapo alisema hadi kukamilika kwa zoezi hilo awamu ya kwanza wanatarajia kufikia nyumba 96,000.



# TISA WATEULIWA KUWANIA UBUNGE WILAYANI SAME




***"Kura yako,haki yako.Jitokeze kupiga Kura"***

Jumla ya wagombea tisa wameteuliwa kugombea ubunge katika majimbo ya Same Mashariki na Same Magharibi kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 29 Mwaka huu.

Akitoa taarifa hiyo Msimamizi wa uchaguzi wa majimbo hayo Bi.Nice Ngasala, amesema kwenye Jimbo la Same Magharibi waliochukua fomu ya Ubunge walikuwa Saba lakini walioteuliwa ni watano ambao ni Dkt. Mathayo David (CCM) Dkt Kidagho Mohamed (AAFP) Bw.Elisante Majid (ACT- Wazalendo) Bi. Ester Maregesi (Chama cha MAKINI) na Gervas Mgonja (CHAUMA ) ambapo Abdul Mkongo (NCCR -Mageuzi) hakurejesha fomu huku Sidra Katanga ( N.R.A) akiwekewa pingamizi.

Kwa upande wa Jimbo la Same Mashariki walioteuliwa kugombea Ubunge ni Deogratias Kweyamba (N.R.A), Bi.Anne Kilango (CCM) Nagy Kaboyoka (ACT-Wazalendo) Bi. Zaina Nampoto ( Chama cha MAKINI) ambapo Allan Alson wa CHAUMMA alichelewa kurejesha fomu hivyo kukosa uteuzi.

Kwa upande wa nafasi za udiwani jumla ya wagombea 39 wameteuliwa kugombea udiwani Jimbo la Same Magharibi lenye Kata 20 huku wagombea 25 wakipitishwa kugombea udiwani Jimbo la Same Mashariki ambalo lina Kata 14.Wagombea udiwani waliopitishwa wanatoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), ACT Wazalendo na CHAUMMA.

Bi.Ngasala amewapongeza wote walioteuliwa kugombea nafasi ya ubunge na udiwani na kuwasihi kufanya kampeni zao kwa kufuata sheria taratibu na kanuni kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2025.

Amewataka pia wananchi kujitokeza katika kampeni hizo ili kusikiliza sera za wagombea na kuweza kufanya maamuzi sahihi wakati wa kupiga Kura.

## **‘TUMIENI VEMA MSAADA WA KISHERIA WA MAMA SAMIA LEGAL AID’**




***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akizindua zoezi la Kampeni ya Msaada wa kisheria ya mama Samia Legal Aid (MSLAC) Wilayani Same.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amewataka wananchi kutumia Kampeni ya Msaada wa Kisheria bure unaotolewa kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ijulikanayo kama Mama Samia Legal Aid Campaign ambao unawasaidia wananchi wenye changamoto zinazohitaji msaada wa kisheria ikiwemo kupatiwa msaada wa mawakili kuwasimamia Mahakamani.

"Wale wote wenye changamoto za kisheria na wale wasio na uwezo wa kuajiri mawakili wa kuwawakilisha mahakamani au kuwaandalia nyaraka za kisheria wafike kuwasilisha changamoto zao mbele ya timu ya msaada wa kisheria"alisema

Amesema kampeni hiyo inatarajiwa kupunguza malalamiko ya kisheria kwa wananchi pamoja na kutoa elimu kwa umma.

Kwa upande wake, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Wakili Upendo Kivuyo, amesema huduma zitakazotolewa katika kampeni hiyo ni pamoja na kusuluhisha migogoro ya ndoa na talaka, migogoro ya ardhi, mirathi, unyanyasaji wa kijinsia, haki za binadamu, pamoja na masuala ya utawala bora.

Aidha, ameeleza kuwa huduma hizo zinatolewa kwa njia ya ushauri, usuluhishi na hata uwakilishi mahakamani pale inapohitajika, ili kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake kwa wakati.

Amesema kwa awamu ya kwanza huduma hiyo ilifika kwenye Kata kumi na kwasasa wanafikia Kata tatu ambazo ni Same,Kisima na Stesheni.

“Hadi sasa tumeweza kufikia wananchi 127 wenye uhitaji mbalimbali ambapo migogoro imesuluhishwa na miwili imefikishwa Mahakamani” alisema Upendo na kuongeza kuwa malalamiko yaliyo mengi ni ya Ardhi na Mirathi.

Kampeni ya msaada wa kisheria bure kwa wananchi (Mama Samia Legal Aid Campaign) iliasisiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2023 kwa lengo la kutoa msaada kwa kisheria kwa wananchi wasio na uwezo wa kuajiri mawakili ambayo inatekelezwa kwa miaka mitatu hadi kufikia mwezi Februari 2026 katika maeneo yote nchini

**“UKITAKA KUFANIKIWA KATIKA KILIMO FUATA KANUNI BORA” NINZAR-AFISA KILIMO SAME**



***Afisa Kilimo na Mifugo (W) Same Bw.Ninzar Idd akizungumza akiwa kwenye maonesho ya nanenane Kanda ya Kaskazini*.**

Afisa Kilimo,Mifugo na Uvuvi Wilayani Same Bw. Ninzari Idd ameshauri Wakulima kufuata kanuni Bora za Kilimo ili kuwawezesha kupata mavuno mengi na hivyo kuwa na Kilimo chenye tija.

Bw.Idd ametoa ushauri huo wakati wa kilele cha Maadhimisho ya nanenane ambapo amesema mkulima akizingatia kuchagua mbegu bora, matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu ni lazima atapata mavuno mengi na yaliyo Bora.

Akiwa katika maonesho ya Kilimo ya Nanenane 2025 Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika Viwanja vya Themi-Njiro Jijini Arusha Bw.Ninzar alisema iwapo wakulima watachagua mbegu bora,watumie mbolea na viuatilifu uwezekano wa kupata mavuno mengi ni mkubwa.

“Unaona kwenye banda letu hili mazao yote yaliyostawishwa hapa yamestawi na yana ubora unaotakiwa na hii ni kwasaababu tumezingatia kanuni bora za kilimo kuanzia wakati wa kupanda mazao haya,usimamizi mzuri wakati wa kuyakuza na hadi sasa yamefikia mavuno” alisema Afisa Kilimo huyo huku akionesha mahindi yaliyostawi vema

Aidha amewataka Wakulima wanapopata changamoto za kilimo kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa maafisa ugani walio kwenye Kata na baadhi ya vijiji Wilayani Same

Bi .Helena Mmari ni Mkulima wa wilayani Arumeru ambaye alitembelea banda la  Same kwenye maonesho hayo na kupata elimu ya ukuzaji bora wa mazao hasa mahindi.

## TABASAMU LA USHINDI…UMITASHUMTA




***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama akipokea vikombe vya ushindi ambavyo Same imejishindia kwenye Mashindano ya UMITASHUMTA 2025,Anayemkabidhi ni Afisa Elimu Msingi (W) Bw.Marclaud Mero***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama (kushoto ) akipokea Vikombe vya Ushindi vya mashindano ya

Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) 2025 toka kwa Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Bw.Marclaud Mero akiwa pamoja Watumishi wa Idara hiyo.

Wilaya ya Same imeshika nafasi ya kwanza kimkoa kwenye mashindano hayo na imejinyakulia Vikombe tisa vya ushindi.

Akitoa taarifa ya ushindi huo kwa Mkurugenzi, Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Mwl.Marclaud Mero alisema Wilaya ya Same imeshika nafasi ya kwanza kwenye mchezo wa Riadha , Goalball Wavulana na Sanaa za maonesho.

Aliitaja michezo mingine iliyoitoa Same kimasomaso kuwa ni pamoja na Basketball, Goalball Wasichana na Volleyball wasichana  na wavulana ambazo zilishika nafasi ya pili kimkoa.

Mpira wa Miguu wasichana walishika nafasi ya tatu na Usafi Wilaya ilishika nafasi ya tatu.

Wilaya pia ilifanikiwa kutoa wanamichezo 31 ambao waliunda timu ya Mkoa na Kushiriki Mashindano hayo Ngazi ya Taifa.

Mkurugenzi ameipongeza Idara ya Elimu Msingi kwa kusimamia vema michezo.



# MATUKIO KATIKA PICHA



***Kaimu Mkurugenzi  Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Wambura Yamo (kushoto) akimkabidhi zawadi Mkulima bora wa Pamba  Bw.Gabriel Mbwambo,Zawadi hiyo imetolewa na Bodi ya Pamba Tanzania.***





***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa  Kasilda Mgeni akimkabidhi cheti cha pongezi baada ya kufanya vizuri kwenye ukusanyaji mapato Mkurugenzi wa Mamlaka ya maji Safi na Usafi wa Mazingira Same-Mwanga (SAMWASA) Mhandisi Rashid Mwinjuma***




**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138, SAME**

**Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Septemba, 2025 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022***